## KUTOA TAARIFA YA UNYANYASAJI WA KIJINSIA & UBAGUZI WA KIJINSIA

Ikiwa unaamini mtoa huduma wa nyumba, mpango wa nyumba, au mkopeshaji aliye na bima ya FHA amekunyima nyumba au anakutendea tofauti kwa sababu ya jinsia, mwelekeo wa kijinsia, au utambulisho wako wa kijinsia, unaweza kuwasilisha malalamiko ya Sheria ya Makazi ya Haki kwa HUD.

Ni muhimu kutosubiri kuchukua hatua; lazima uwasilishe malalamiko yako ndani ya mwaka mmoja baada ya tarehe ya mwisho ya madai ya ubaguzi au unyanyasaji wa kijinsia.

Malalamiko ya Sheria ya Makazi ya Haki yanaweza kuwasilishwa:

- Mtandaoni kwenye hud.gov/fairhousing
- Kwa simu kwa 1-800-669-9777 au 1-800-877-8339 (TTY)

Ni kinyume cha sheria kwa mtoa huduma ya makazi kukulipizia kisasi kwa kuwasilisha malalamiko au kushiriki katika mchakato wa malalamiko ya HUD. Ikiwa unaamini umelipizwa kisasi kwa kutoa taarifa ya unyanyasaji wa kijinsia au kitendo cha ubaguzi, wasiliana na HUD.


## JE, UNAHITAJI KUWASILISHA MALALAMIKO YA SHERIA YA MAKAZI YA HAKI?

Wasiliana na HUD kwa 1-800-669-9777 au 1-800-877-8339 (TTY) au tembelea hud.gov/fairhousing

## JE, UNA MASWALI ZAIDI KUHUSU SHERIA YA MAKAZI YA HAKI NA UBAGUZI WA KIJINSIA?

Ongea na wakili **bila malipo** kwa kupiga simu ya Ushauri wa Makazi ya Msaada wa Kisheria wa Idaho kwa **208-746-7541** (TRS, piga 7-1-1). Jumatatu - Ijumaa 4 asubuhi - 9:30 alasiri MT.

Au tuma ombi mtandaoni kwa **idaholegalaid.org.**



**Kwa maelezo zaidi kuhusu haki zako za Sheria ya Makazi ya Haki:**
**hud.gov/fairhousing**
**idaholegalaid.org**
**ifhcidaho.org**
**Simu ya Ushauri wa Makazi: 208-746-7541**

Kazi ambayo ilitoa msingi wa chapisho hili ilifadhiliwa na fedha za ruzuku za Idara Makazi na Maendeleo ya Mji. Chapisho na matokeo ya kazi hii yamekabidhiwa kwa umma. Mwandishi na mchapishaji wanawajibika tu kwenye usahihi wa taarifa na tafsiri zilizomo kwenye chapisho hili. Tafsiri hizo sio lazima ziakisi maoni ya Serikali ya Kuu.

# Makazi ya Haki: Ubaguzi wa Kijinsia



Idaho Legal Aid Services, Inc.

## SHERIA YA MAKAZI YA HAKI

Sheria ya Makazi ya Haki inakataza ubaguzi katika uuzaji na upangishaji wa nyumba kulingana na madaraja yafuatayo yanayolindwa: Kabila, Rangi, Jinsia, Dini, Asili ya Kitaifa, Ulemavu, au Hali ya Familia. Sheria ya Makazi ya Haki ilipitishwa kama sehemu ya Sheria ya Haki za Kiraia ya 1968.

Unaweza kupata maelezo zaidiuji kuhusu vitendo ambavyo vinaweza kukiuka Sheria ya Makazi ya Haki kwa kutembelea: https://www.hud.gov/program_offices/fair_housing_equal_opp.

Sheria ya Makazi ya Haki inafanya iwe kinyume cha sheria kubagua katika makazi kwa msingi wa jinsia. **Ubaguzi wa kijinsia** unaweza kujitokeza katika njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na: ubaguzi dhidi ya wanawake, ubaguzi dhidi ya wanaume, ubaguzi dhidi ya mtu kwa sababu hakubaliani na kanuni zinazojulikana za kijinsia zinazohusiana na mwelekeo wa kingono au utambulisho kijinsia, na ubaguzi unaotokana na unyanyasaji wa kijinsia katika nyumba.




### Ubaguzi wa Kijinsia

Watoa huduma za makazi na wakopeshaji watakuwa wanajihusisha na ubaguzi haramu wa kijinsia ikiwa watamtendea mtu fulani tofauti kwa sababu ya jinsia yake.

Mifano ya Vitendo vya Ubaguzi:

- Kukataa kumpangisha mtu kwa sababu ya jinsia yake.
- Kutangaza upendeleo wa kijinsia, kama vile “Kukubali maombi kutoka kwa wanaume pekee” (Hata hivyo, kuna mazingira yanayoruhusu upendeleo wa kijinsia wakati wa kutangaza nyumba ambayo watu wataishi pamoja).
- Kumfukuza mtu kwenye makazi kwa sababu yeye ni mwathirika wa unyanyasaji wa majumbani.

### Mwelekeo wa Kingono na Utambulisho wa Kijinsia

Februari ya 2021 Idara ya Makazi na Maendeleo ya Miji ya Marekani (HUD) ilitangaza kwamba itatekeleza Sheria ya Makazi ya Haki ili kuzuia ubaguzi kwa misingi ya mwelekeo wa kingono na utambulisho wa kijinsia (pamoja na ubaguzi unaotokana na kutofuata kanuni za kijinsia).

Zaidi ya hayo, Sheria ya Usawa ya HUD inataka matumizi sawa ya mipango inayofadhiliwa na HUD bila kujali mwelekeo wa kingono wa mtu, utambulisho wa kijinsia, au hali ya ndoa.

Mifano ya Vitendo vya Ubaguzi:

- Mwanamke aliyebadilisha jinsia kuambiwa asivae mavazi ya wanawake katika maeneo ya kawaida ya nyumba yake.
- Mtoa huduma ya makazi kuuliza juu ya mwelekeo wa kijinsia au utambulisho wa kijinsia wa mpangaji katika kuamua ustahiki wao kwenye makazi.
- Mdhamini wa mkopeshaji mwenye bima ya FHA kukataa ombi la mkopo kwa wanaume wawili kwa sababu anadhani ni wapenzi wa jinsia moja.

### Unyanyasaji wa Kijinsia

Unyanyasaji wa kijinsia katika makazi ni aina ya ubaguzi wa kijinsia hivyo unakiuka Sheria ya Makazi ya Haki. Kuna aina mbili za unyanyasaji wa kijinsia: 1) nipe nikupe na 2) mazingira ya uhasama.

Unyanyasaji wa Nipe Nikupe hufanyika wakati mtoa huduma ya makazi anaomba kufanya ngono kama masharti za huduma zinazohusiana na makazi. Mifano ya Unyanyasaji wa Nipe Nikupe:

- Mmiliki wa nyumba kuomba afanye ngono na mpangaji badala ya malipo ya kodi
- Msimamizi wa nyumba kumfukuza mpangaji ambaye amekataa kutoa rushwa ya ngono

Unyanyasaji wa mazingira ya uhasama unatokea pale mpangaji anapofanyiwa vitendo vibaya na visivyofaa vya kingono.
Mifano ya Unyanyasaji wa Mazingira ya Uhasama:

- Mwenye nyumba kukushikashika, kukubusu au kupapasa kusikokubalika mara kwa mara
- Msimamizi wa nyumba kuwa na mazoea ya kusema maneno yasiyofaa kuhusu mwili wa mpangaji